BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 23 Mei, 2025
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

217. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kiasi gani Tume ya Haki za Binaadamu inasimamia suala zima la misingi ya utawala bora isikiukwe nchini mwetu.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

23. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kifungu cha 23 cha Sheria ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005 kinataka miradi yote ya maendeleo inayofanyika Zanzibar iwe imesajiliwa na Wakala wa Usalama na Afya Kazini, na mapato ya usajili huu huingia moja kwa moja Serikalini.

(a) Je, ni miradi mingapi ya maendeleo ambayo imesajiliwa na Idara Usalama na Afya Kazini.

(b) Je, ni mapato ya kiasi gani yamepatikana kutokana na usajili huo wa miradi ya maendeleo.

(c) Je, ni kwa namna gani Idara ya Usalama na Afya Kazini inaifikia sekta isiyo rasmi Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

276. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na tatizo kubwa la maradhi ya kupooza katika jamii zetu.

Je, tathmini ya maradhi hayo iko vipi kwa sasa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

219. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kiasi gani Mtaala Mpya wa Umahiri utaweza kufungua fursa za ufundi kwa vijana.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

135. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Visiwa vya Unguja na Pemba vinapata umeme kupitia waya za baharini zenye uwezo wa megawati 100 na megawati 45 za mkondo wa kilovoti 132 kwa Unguja na megawati 20 za mkondo wa kilovoti 33 kwa Pemba kutoka gridi ya Taifa ya Tanzania bara.

(a) Kwa kuwa kiwango cha umeme kinachopatikana kinatosheleza matumizi yetu, je kuna sababu gani kwa sasa za umeme kuzimwa mara kwa mra.

(b) Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu sasa, je, Serikali inawaeleza nini wananchi juu ya kuondokana na tatizo hili.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
23 Mei, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR